**MAELEZO YA UTANGULIZI YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MH. JAJI WA RUFAA MST. SEMISTOCLES S. KAIJAGE WAKATI WA KUWASILISHA TAARIFA YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020 KWA MHE. SAMIA S. HASSAN RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TAREHE 21 AGOSTI, 2021 IKULU, DAR ES SALAAM**

***Mheshimiwa Rais;***

Awali ya yote ninamshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia uhai na kutuwezesha kufikia siku ya leo. Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekamilisha mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kuandaa na sasa kuwasilisha kwako taarifa ya uchaguzi. Aidha, Tume inatoa shukrani za dhati kwako Mheshimiwa Rais kwa kukubali kukutana nasi.

Kwa kuwa Tume inakutana na wewe kwa mara ya kwanza tangu kutokea msiba mkubwa, wa kumpoteza aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wa awamu ya tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; Tume inatoa pole kwako binafsi, kwa familia, Serikali, na wananchi wote kwa ujumla.

Aidha, Tume inakupongeza Mhe. Rais kwa kuweza kuipitisha nchi katika kipindi hicho kigumu kwa Amani na utulivu.

***Mheshimiwa Rais;***

Baada ya kutoa utangulizi huo, sasa nianze kuwasilisha yaliyomo katika taarifa hii kwa kuelezea, kwa ufupi, juu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa mujibu wa ibara ya 74(6) na ibara ya 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, zikisomwa pamoja na kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina majukumu yafuatayo-

a) Kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano;
b) Kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge;
c) Kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge;
d) Kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi wa Madiwani;
e) Kuteua na kuwatangaza Wabunge Wanawake Viti Maalum;

f) Kuteua na kuwatangaza Madiwani Wanawake Viti Maalum; na
g) Kutoa elimu ya mpiga kura nchini kote; kuratibu na kusimamia watu na taasisi zote zinazoendesha elimu hiyo.

*Mheshimiwa Rais;*

Ibara ya 74(1) na (2) ya Katiba imetaja muundo wa Tume na uteuzi wa Wajumbe wake ambao ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe. Vilevile, Katiba imeainisha kwamba, kila Mjumbe wa Tume anatumikia madaraka yake katika kipindi cha miaka mitano. Eneo lingine ambalo limeelezwa katika Katiba ni kwamba, Tume katika utekelezaji wa majukumu yake, itakuwa ni idara huru inayojitegemea, itafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao, na kwamba mtendaji wake mkuu ni Mkurugenzi wa Uchaguzi.

*Mheshimiwa Rais;*

Kama ambavyo nimeeleza hapo awali, Tume iko hapa leo kwa lengo la kuwasilisha kwako taarifa ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, ikiwa ni ishara ya kukamilika kwa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Taarifa hii imegawanyika katika sura kumi na mbili (12), ambazo zinaonesha utekelezaji wa hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi,

kuanzia maandalizi ya bajeti, uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, upangaji wa ratiba ya uchaguzi mkuu na kalenda ya matukio, uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, kuhesabu na kujumlisha kura na hatimaye kutangaza matokeo. Aidha, taarifa hii, imegusia elimu ya mpiga kura na ushirikishwaji wa wadau. Pia, taarifa imeainisha mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika mchakato wa uchaguzi, pamoja na maoni na mapendekezo.

***Mheshimiwa Rais;***

Tume katika kipindi cha uchaguzi ilifanya maandalizi ya bajeti kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza, ilikuwa ni bajeti kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ambapo jumla ya Shilingi 154,313,824,607.88 zilitumika katika zoezi hilo. Fedha hizo, pamoja na mambo mengine, zilitumika kugharamia ununuzi wa vifaa vya uboreshaji, uhuishaji wa mifumo ya uchaguzi, uchapishaji wa nyaraka mbalimbali, mafunzo kwa watendaji wa uboreshaji na utoaji wa elimu ya mpiga kura.

Awamu ya pili ilikuwa ni bajeti ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, ambapo kiasi cha Shilingi 262,493,380,671.00 zilitumika kuendesha zoezi hilo. Fedha hizi nazo zilitumika katika kugharamia shughuli mbalimbali za uchaguzi ikiwemo, ununuzi wa vifaa na huduma kama vile karatasi za

kura, vituturi, masanduku ya kura, uchapishaji wa nyaraka mbalimbali, mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi na elimu ya mpiga kura.

Kwa mujibu wa kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kikisomwa pamoja na kifungu cha 120 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, fedha zilizotumika katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, zililipwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Aidha, kwa mara ya kwanza Serikali imeweza kugharamia shughuli zote kuanzia uboreshaji wa Daftari hadi uchaguzi mkuu kwa asilimia mia moja bila kutegemea misaada.

***Mheshimiwa Rais;***

Uchaguzi ni mchakato na si tukio. Unapokamilika uchaguzi mmoja, tayari maandalizi kwa ajili ya uchaguzi Mkuu mwingine yanaanza. Kwa mfano kuelekea uchaguzi mkuu uliopita, pamoja na mambo mengine, Tume ilianza na zoezi la utambuzi wa maeneo ya kiutawala na uhakiki wa vituo vya kuandikishia wapiga kura. Zoezi hilo liliiwezesha Tume kutambua uwepo wa halmashauri 184 kwa upande wa Tanzania Bara na wilaya 11 kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Kata 3,956 za Tanzania Bara na Shehia 388 za Tanzania Zanzibar.

Baada ya kukamilisha zoezi la utambuzi wa maeneo ya kiutawala, Tume mwaka 2018 ilifanya uhakiki wa vituo vya kuandikishia wapiga kura. Lengo la uhakiki huo, lilikuwa ni kuona kama vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, bado vilikuwa na hadhi na sifa ya kuwa vituo vya kuandikishia wapiga kura kwa mujibu wa sheria. Lengo lingine lilikuwa ni kuona iwapo kuna uhitaji wa kuongeza vituo kwa maeneo ambayo yanakidhi vigezo.

Matokeo ya zoezi hilo la uhakiki yalionesha kuwa, baadhi ya vituo vya kuandikisha wapiga kura vilikuwa vimepoteza sifa na hivyo vilihamishiwa katika maeneo stahiki. Vituo vingine vilifanyiwa marekebisho ya majina na maeneo yaliyokuwa na uhitaji yaliongezewa vituo. Kutokana na hatua hiyo, vituo vya kuandikishia wapiga kura viliongezeka kutoka vituo 36,929 vilivyotumika kuandikishia wapiga kura mwaka 2015 hadi vituo 37,814 vilivyotumika kuandikisha wapiga kura mwaka 2020.

***Mheshimiwa Rais;***

Baada ya kukamilika kwa zoezi hilo la uhakiki wa vituo, Tume iliendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kwa mujibu wa sheria. Zoezi hili ni muhimu kwani huonyesha utayari wa wananchi katika kushiriki michakato ya uchaguzi kwa kujiandikisha ama kuboresha taarifa zao katika Daftari. Inafahamika kuwa ili mwananchi

aweze kupiga kura siku ya uchaguzi ni lazima awe amejiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Zoezi la uboreshaji wa Daftari lilizinduliwa rasmi tarehe 18 Julai, 2019 mkoani Kilimanjaro na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa. Baada ya uzinduzi huo, zoezi la uboreshaji wa Daftari liliendelea katika maeneo mengine nchi nzima na kukamilika tarehe 20 Juni, 2020.

Walengwa wa zoezi hilo, kwa mujibu wa sheria walikuwa ni wapiga kura wapya, waliotimiza umri wa miaka 18 na kuendelea na wale waliotarajiwa kutimiza umri huo kabla au siku ya uchaguzi, wale waliohama kata au majimbo, na wale waliopoteza au kadi zao kuharibika. Vivyo hivyo, zoezi hilo lililenga kuwaondoa kwenye Daftari wapiga kura waliopoteza sifa kwa mujibu wa sheria.

Matokeo ya zoezi la uboreshaji wa Daftari yalionesha kuwa idadi ya wapiga kura iliongezeka kutoka jumla ya wapiga kura 23,161,440 wa mwaka 2015 hadi wapiga kura 29,754,699 kwa mwaka 2020. Hili ni ongezeko la wapiga kura 6,593,259 sawa na asilimia 28.47. Uchambuzi wa Tume katika eneo hili uliangalia pia uwiano wa kijinsia ambapo takwimu za wapiga kura walioandikishwa zinaonesha wanaume ni 14,768,719 na wanawake 14,985,980. Kwa ujumla, vijana wenye umri wa miaka 18 hadi

35 walioandikishwa ni 15,986,695. Vilevile, takwimu zinaonesha kuwa wapiga kura 13,211 wenye ulemavu wa macho, mikono na ulemavu wa aina nyingine waliandikishwa.

***Mheshimiwa Rais;***

Maandalizi mengine yaliyofanywa na Tume kabla ya uchaguzi mkuu yalihusu kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020. Katika kuandaa kanuni hizo, Tume ilishirikisha wadau wa uchaguzi vikiwemo vyama vya siasa kwa njia ya maandishi na mikutano, lengo likiwa ni kuwa na uelewa wa pamoja na kupata maoni yao. Pamoja na kanuni hizo, Tume pia iliandaa maelekezo kwa watendaji na wadau wa uchaguzi, mwongozo wa kutoa elimu ya mpiga kura na mwongozo wa watazamaji wa uchaguzi.

Hatua nyingine muhimu katika mchakato wa uchaguzi ilikuwa ni kupanga na kutangaza ratiba ya uchaguzi mkuu. Tume ilipanga ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kuzingatia masharti ya uteuzi yaliyomo katika kifungu cha 37 (1) (a) cha Sheria ya Taifa Uchaguzi. Kwa mujibu wa kifungu tajwa, Tume inatakiwa kupanga siku ya uteuzi kuwa si chini ya siku tano na si zaidi ya siku 25 baada ya kuvunjwa kwa Bunge. Kwa kuzingatia masharti hayo na tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge ambayo

ilikuwa tarehe 31 Julai, 2020, Tume iliandaa na kutangaza Ratiba ya Uchaguzi Mkuu. Ratiba hiyo ilionesha kuwa uteuzi wa wagombea ni tarehe 25 Agosti, 2020, kampeni kuanza tarehe 26 Agosti, hadi tarehe 27 Oktoba, 2020 kwa upande wa Tanzania Bara na tarehe 26 Oktoba, 2020 kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Ratiba ya uchaguzi ilitolewa kwa umma kupitia vyombo vya habari na ilichapishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kupitia tangazo Na. 532 la tarehe 17 Julai, 2020.

Wakati Tume inatangaza ratiba ya uchaguzi, tayari ilikuwa imeandaa ratiba ya utekelezaji ambayo ilionesha hatua muhimu za uchaguzi ikiwemo uteuzi wa wagombea, kampeni, usafirishaji wa vifaa, usajili wa watazamaji, elimu ya mpiga kura, mafunzo kwa watendaji, uundaji wa kamati mbalimbali za uchaguzi, upigaji kura, kuhesabu na kujumlisha kura na hatimaye kutangaza matokeo.

Maandalizi pia yalihusu ununuzi na usambazaji wa vifaa vyote vilivyohitajika, uteuzi wa watendaji wa uchaguzi ngazi ya mkoa na halmashauri, uteuzi wa wasimamizi wa vituo na wasaidizi wao, na makarani waongozaji wapiga kura kwa kila kituo. Watendaji wote walipatiwa mafunzo stahiki yaliyotolewa na Tume.

*Mheshimiwa Rais;*

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi, tarehe 25 Agosti, 2020 ilikuwa siku ya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Kwa upande wa kiti cha Rais, vyama vya siasa 17 kati ya vyama 19 vyenye usajili wa kudumu vilipendekeza na kuwadhamini wagombea kuwania nafasi ya kiti cha Rais. Kati yao, Tume iliwateua wagombea 15 kuwania nafasi hiyo.

Pamoja na kuwepo kwa changamoto ya ushiriki mdogo wa wanawake katika michakato ya uchaguzi, hasa eneo la uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa, idadi ya wanawake waliojitokeza na kupendekezwa na vyama vyao, kugombea nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais iliongezeka kutoka wanawake wawili mwaka 2015 hadi wanawake 7 kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais ulienda sambamba na ule wa Wabunge na Madiwani. Katika nafasi ya Ubunge jumla ya Wagombea 1,257 waliteuliwa, kati yao wanawake ni 293 wanaume ni 964. Kwa nafasi ya Udiwani, jumla ya wagombea 9,231 waliteuliwa, kati yao wanawake ni 668 na wanaume ni 8,563.

Aidha, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, wagombea Ubunge 28 na Madiwani 882 walichaguliwa bila kupingwa. Kwa mujibu wa kifungu cha

44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na kifungu cha 45(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, endapo mpaka muda wa uteuzi unapokamilika ni mgombea mmoja tu ameteuliwa inachukuliwa kuwa amechaguliwa bila kupingwa.

***Mheshimiwa Rais;***

Sheria za uchaguzi na kanuni zake zimeweka taratibu na mamlaka za kushughulikia malalamiko yanayojitokeza katika kila hatua ya mchakato wa uchaguzi. Wakati wa uteuzi wa wagombea Ubunge na Udiwani sheria na kanuni za uchaguzi zimeweka utaratibu wa kuweka pingamizi na kuwasilisha malalamiko kwa msimamizi wa uchaguzi. Hii hutokea endapo mgombea anaona kuwa mgombea mwingine hajakidhi sifa za kisheria. Iwapo muweka au muwekewa pingamizi katika ngazi ya Udiwani na Ubunge hakuridhika na maamuzi ya msimamizi wa uchaguzi anaweza kukata rufaa kwenye Tume. Kwa upande wa kiti cha Rais, pingamizi zinawasilishwa Tume na kufanyiwa uamuzi.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilipokea pingamizi mbili ambazo ziliwasilishwa dhidi ya wagombea wa kiti cha Rais. Baada ya Tume kupitia pingamizi hizo na kujiridhisha kuwa hazikuwa na msingi wa kisheria, ilizikataa. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo walipokea na kuzifanyia kazi jumla ya

pingamizi 334 dhidi ya wagombea Ubunge. Wale ambao hawakuridhika na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi, walipaswa kukata rufaa kwenye Tume.

***Mheshimiwa Rais***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea, ilisikiliza na kuzitolea uamuzi jumla ya rufaa 165 za wagombea Ubunge. Rufaa 67 kati ya 98 sawa na asilimia 68 zilizoomba wagombea kurejeshwa katika orodha ya wagombea zilikubaliwa. Aidha, rufaa 31 sawa na asilimia 22 ya rufaa zilizoomba wagombea kurejeshwa katika orodha ya wagombea zilikataliwa. Kati ya rufaa 67 zilizoomba kuondolewa kwa wagombea ambao walikuwa wameteuliwa katika majimbo, ni rufaa tatu sawa na asilimia 4.5 zilizokubaliwa. Hivyo, rufaa 64 sawa na asilimia 95.5 zilikataliwa na wagombea waliendelea kugombea Ubunge.

Kwa upande wa Madiwani, wasimamizi wa uchaguzi walipokea na kufanyia uamuzi jumla ya pingamizi 1,228. Wale ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa walitakiwa kukata rufaa kwenye Tume.  Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea, ilisikiliza na kuzitolea uamuzi jumla ya rufaa 451 za wagombea Udiwani. Rufaa 235 kati ya rufaa 389 sawa na asilimia 60.41 ambazo wagombea waliomba warejeshwe kwenye orodha ya wagombea

zilikubaliwa. Aidha, rufaa 154 kati ya 389 sawa na alimia 39.59 ambazo wagombea waliomba warejeshwe kwenye orodha ya wagombea zilikataliwa. Vilevile, rufaa zote 62 ambazo warufani waliomba wagombea waondolewe kwenye orodha ya wagombea zilikataliwa na wagombea waliendelea kuwemo kwenye orodha ya wagombea wa Udiwani.

***Mheshimiwa Rais;***

Changamoto iliyojitokeza katika eneo hili ni kuwepo kwa malalamiko kwa baadhi ya vyama vya siasa na wagombea kuwa hawakupata matokeo ya rufaa zao ambazo kimsingi hazikuwahi kupokelewa wala kusajiliwa na Tume. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, rufaa zote ambazo Tume ilizipokea ilizifanyia kazi na kutoa uamuzi kama nilivyokwisha kueleza.

Kukamilika kwa zoezi la uteuzi wa wagombea kulifuatiwa na kampeni za uchaguzi. Kama tunavyofahamu, kampeni zilianza tarehe 26 Agosti, 2020 na kuisha tarehe 27 Oktoba, 2020 kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar kampeni zilimalizika tarehe 26 Oktoba, 2020 ili kupisha upigaji kura wa mapema. Kampeni hizi zilifanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya hadhara, nyumba kwa nyumba, mabango, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Kampeni hizo, pamoja na mambo mengine, zilihusisha kunadi wagombea na kuelezea sera, ilani za uchaguzi na kuwahamasisha wapiga kura kujitokeza kwa

wingi siku ya uchaguzi. Kwa ujumla, na katika maeneo yaliyo mengi ya uchaguzi, kampeni ziliendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni, maadili na taratibu zilizowekwa.

Aidha, maeneo ambako kulikuwa na malalamiko kuhusiana na ukiukwaji wa maadili ya uchaguzi kamati za maadili katika ngazi husika zilishughulikia malalamiko hayo.

***Mhesimiwa Rais;***

Michakato mbalimbali ya uchaguzi ilitufikisha siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba, 2020 ambayo ilikuwa ni siku ya kupiga kura. Serikali ilitangaza siku hiyo ya Jumatano kuwa ni siku ya mapumziko na hii ilikuwa ni mara ya kwanza uchaguzi kufanyika siku ya katikati ya wiki. Hatua hiyo ilitokana na maoni na mapendekezo ya muda mrefu ya wadau wa uchaguzi walioshauri kwamba siku za ibada zisitumike kwa shughuli za uchaguzi mkuu. Vituo vilifunguliwa kuanzia 1:00 asubuhi hadi 10:00 jioni. Zoezi hilo lilifanyika katika vituo vya kupigia kura 81,567 nchi nzima.

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kikisomwa pamoja na kifungu cha 58 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, vyama vya siasa vilikuwa na haki na wajibu wa kuweka mawakala katika vituo vya kupigia kura kwa lengo la kushuhudia na

kufuatilia hatua zote za upigaji kura kituoni. Wakati wa kupiga kura, kipaumbele kilitolewa kwa watu wenye ulemavu, wazee, wagonjwa, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga.

***Mheshimiwa Rais;***

Baada ya upigaji kura kukamilika, vituo hivyo vilitumika kuhesabia kura. Mchakato wa kuhesabu kura vituoni ulipokamilika, nakala za fomu za matokeo zilibandikwa sehemu za wazi nje ya vituo husika. Fomu za matokeo na vifaa vya uchaguzi vilipelekwa kwa wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo na kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa kata kwa ajili ya majumuisho ya kura.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, wapiga kura waliojitokeza kupiga kura ni 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 kati ya wapiga kura 29,754,699 waliojiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Zoezi la kujumlisha kura za uchaguzi wa Rais lilifanyika kwanza katika ngazi ya jimbo ambapo wasimamizi wa uchaguzi baada ya kupokea matokeo hayo kutoka vituoni yalijumuishwa katika fomu moja maalum ambayo ilitumwa kituo cha majumuisho ya kura za Rais. Baada ya kupokelewa yalihakikiwa na kutangazwa kama matokeo ya awali mbele ya wale wanaoruhusiwa, kwa mujibu wa sheria, kuwepo katika maeneo ya

kujumlisha na kutangaza matokeo wakiwemo mawakala wa vyama vya siasa na watazamaji wa uchaguzi.

Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (*Results Management System* - RMS) uliwezesha kupatikana kwa jumla ya kura zote zilizopigwa na idadi ya kura alizopata kila mgombea wa kiti cha Rais katika jimbo husika. Matokeo ya uchaguzi wa Rais yalitangazwa ndani ya saa 48 baada ya kukamilika kwa zoezi la kupiga kura. Tume kwa mamlaka iliyopewa na Katiba, ilimtangaza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa mgombea wa CCM kuwa mshindi wa kiti cha Rais na aliyekuwa mgombea mwenza Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa mshindi wa kiti cha Makamu wa Rais kwa kupata kura 12,516,252 ambazo ni sawa na asilimia 84.4 ya kura zote zilizopigwa.

***Mheshimiwa Rais;***

Zoezi la kujumlisha na kutangaza matokeo katika majimbo lilisimamiwa na kuendeshwa na wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo. Wasimamizi waliwatangaza washindi wa Ubunge katika majimbo husika. Matokeo hayo yanaonesha kwamba kati ya majimbo 264, chama cha ACT-Wazalendo kilishinda katika majimbo manne sawa na asilimia 1.51; CCM majimbo 256 sawa na asilimia 96.97; CHADEMA jimbo moja sawa na asilimia 0.38; CUF majimbo matatu sawa na asilimia 1.14. Wasimamizi

wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata walisimamia zoezi la kujumlisha kura za uchaguzi za Madiwani, na hatimaye kuwatangaza washindi wa nafasi za Udiwani katika kata husika.

Matokeo ya jumla ya uchaguzi wa Madiwani yalionesha kwamba kati ya kata 3,952 zilizoshiriki katika uchaguzi wa Madiwani, Chama cha ACT-Wazalendo kilipata Madiwani 22 sawa na asilimia 0.56; CCM Madiwani 3,819 sawa na asilimia 96.63; CHADEMA madiwani 85 sawa na asilimia 2.15; CUF Madiwani 20 sawa na asilimia 0.51; DP Diwani mmoja sawa na asilimia 0.03; na NCCR-Mageuzi Madiwani watano, sawa na asilimia 0.13.

***Mheshimiwa Rais;***

Eneo lingine muhimu katika michakato ya uchaguzi ni elimu ya mpiga kura ambayo lengo lake ni kumjengea uwezo mpiga kura wa kuweza kushiriki michakato ya uchaguzi. Njia mbalimbali zilitumika kutoa elimu ya mpiga kura ikiwemo vyombo vya habari, mikutano na wadau, gari la elimu ya mpiga kura la Tume, machapisho pamoja na kufanya uchaguzi wa mfano (*mock election*) kwa waandishi wa habari.

Katika eneo hili, Tume pia ilishirikisha taasisi na asasi za kiraia kwa kuzipatia kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura, ambapo wakati wa

uboreshaji wa Daftari kulikuwa na taasisi na asasi 28 na wakati wa uchaguzi mkuu taasisi na asasi za kiraia 252 zilipatiwa vibali.

***Mheshimiwa Rais;***

Ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika mchakato wa uchaguzi umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya uchaguzi mkuu uliopita. Wadau wanaozungumziwa ni pamoja na Serikali, vyama vya siasa, viongozi wa taasisi za dini, vyombo vya habari, taasisi na asasi za kiraia, makundi maalum katika jamii ambayo ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, bila kusahau wazee wa kimila na wazee maarufu.

Wadau hao tumeshirikiana nao kupitia mikutano kuanzia ngazi ya Taifa hadi mkoa kwa nchi nzima, kuwapatia nyaraka mbalimbali zikiwemo sheria, kanuni, maelekezo na miongozo mbalimbali ya uchaguzi. Kwa wadau wengine mfano vyama vya siasa walipata nafasi ya kuwa wajumbe wa kamati mbalimbali za ushauri wakati wa uchaguzi.

Kundi lingine muhimu la wadau wa uchaguzi ni watazamaji wa uchaguzi. Kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka jana, Tume ilitoa mwaliko kwa watazamaji wa ndani na wa kimataifa. Jumla ya taasisi na asasi za ndani 97 zenye jumla ya watazamaji 5,297 na taasisi za kimataifa 17 zenye jumla ya watazamaji 199 zilipewa vibali kwa ajili ya kutazama shughuli za uchaguzi

mkuu. Baada ya uchaguzi mkuu, baadhi ya watazamaji hao wamewasilisha taarifa zao yakiwemo maoni na mapendekezo.

***Mheshimiwa Rais;***

Ibara ya 26 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeainisha haki kwa kila mtu, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, kuchukua hatua za kisheria katika kuhakikisha hifadhi ya katiba na sheria za nchi.

Sheria za uchaguzi zinatoa haki ya kupinga matokeo ya Ubunge na Udiwani kwa kufungua kesi Mahakamani baada ya matokeo kutangazwa. Kifungu cha 111 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na kifungu cha 110 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, vimewataja watu wanaoruhusiwa kupinga matokeo ya uchaguzi Mahakamani. Watu hao ni-

(i) mtu ambaye alipiga kura au alikuwa ana haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaolalamikiwa;

(ii) mtu ambaye alikuwa na haki ya kuteuliwa kuwa mgombea au kuchaguliwa katika uchaguzi huo;

(iii) mtu ambaye alikuwa mgombea katika uchaguzi huo; au

(iv) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa mujibu wa vifungu tajwa vya sheria, baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 wale ambao hawakuridhika na mchakato wa uchaguzi walifungua

kesi Mahakamani, ambapo kesi 4 zinahusu kupinga matokeo ya Ubunge na kesi 11 zinahusu kupinga matokeo ya Udiwani. Ufafanuzi wa kina wa wale ambao hawakuridhishwa na mchakato wa uchaguzi na ambao walitumia haki yao ya kikatiba na kisheria ya kupinga matokeo ya uchaguzi kwa kufuata utaratibu wa kisheria uliowekwa, upo ndani ya kijitabu cha Taarifa ambacho kitakabidhiwa hivi punde.

***Mheshimiwa Rais;***

Katika kusimamia, kuratibu na kuendesha zoezi la uboreshaji wa Daftari la kudumu la wapiga kura na uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, kulikuwa na mafanikio kadhaa. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na

(i) Kufanikisha shughuli hizi katika mazingira magumu ya uwepo wa ugonjwa wa COVID - 19.
(ii) Kuboresha Daftari la kudumu la wapiga kura kufikisha idadi ya wapiga kura 29,754,699 kutoka wapiga kura 23,161,440 walioandikishwa mwaka 2015.
(iii) Kuongeza vituo vya kupigia kura kutoka 65,105 vya mwaka 2015 hadi kufikia vituo 81,567 kwa mwaka 2020.
(iv) Kujenga na kutumia mifumo ya TEHAMA na menejimenti iliyosanifiwa na kujengwa na wataalam wa ndani ya nchi katika usajili wa wagombea, usajili wa watazamaji, uhakiki wa taarifa za wapiga kura na vituo, kujumlisha na kutangaza matokeo.

(v) Kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais ndani ya saa 48 baada ya kukamilika kwa zoezi la kupiga kura.

(vi) Kwa mara ya kwanza, tangu kuanza chaguzi za ushindani wa vyama vingi mwaka 1995, Serikali kugharamia ngazi zote za uchaguzi mkuu kwa asilimia mia moja.

***Mheshimiwa Rais;***

Pamoja na mafanikio hayo, kulikuwa na changamoto kadhaa. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na-

(i) Mlipuko wa ugonjwa wa COVID - 19 wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la kugumu la wapiga kura awamu ya pili na wakati wa hatua nyingine zote za uchaguzi zilizofuata.

(ii) Kuharibika miundo mbinu ya barabara kulikotokana na uwepo wa mvua nyingi hivyo kuathiri usafirishaji na usambazaji wa vifaa vya uboreshaji wa Daftari la kudumu la wapiga kura katika baadhi ya maeneo.

(iii) Kuwepo kwa idadi kubwa ya wananchi waliopoteza kadi za kupigia kura au kadi zao kuharibika.

(iv) Mwitikio mdogo wa wapiga kura katika baadhi ya maeneo.

(v) Baadhi ya asasi na taasisi zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura kushindwa kutoa elimu hiyo.

(vi) Madai ya baadhi ya mawakala wa vyama vya siasa katika baadhi ya maeneo ya uchaguzi kuzuiliwa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura.

***Mheshimiwa Rais;***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliendesha zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama nilivyosema awali. Ili kuboresha zaidi shughuli za uendeshaji wa uchaguzi siku zijazo wadau wa uchaguzi pamoja na Tume wanapendekeza, pamoja na mambo mengine, haya yafuatayo-

(i) Kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Uchaguzi ambayo itaiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.
(ii) Kuwe na watendaji wa Tume hadi ngazi za halmashauri.
(iii) Mamlaka husika ziangalie uwezekano wa kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hizo.
(iv) Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu usimamiwe na mamlaka moja.
(v) Sheria za Uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili.

(vi) Serikali iangalie uwezekano wa kuziwezesha kifedha asasi na taasisi zinazotoa elimu ya mpiga kura katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi.

(vii) Wagombea ubunge na udiwani wanaopita bila kupingwa wapigiwe kura

***Mheshimiwa Rais;***

Kabla ya kuhitimisha maelezo haya, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wale wote waliofanikisha mchakato mzima wa uchaguzi nikianza na Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji wa Rufaa (Mst.) Mbarouk S. Mbarouk, Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wa Tume; Mhe Jaji (Mst.) Mary H. C. S. Longway; Mhe Asina A. Omari; Mhe Jaji (Mst.) Thomas B. Mihayo na Mhe Balozi Omar R. Mapuri. Menejimenti na wafanyakazi wote wa Tume wa kudumu na wa muda wakiongozwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi Dkt. Wilson M. Charles.

Tume pia inawashukuru watendaji wote wa uchaguzi kuanzia waratibu wa uchaguzi wa mikoa, wasimamizi wa uchaguzi na wasaidizi wao ngazi ya jimbo na kata, watendaji katika vituo vya kupigia kura na maafisa wengine wote katika halmashauri waliofanya kazi za uchaguzi.

Aidha, tunatoa shukrani kwa wizara, taasisi na idara za serikali zilizotoa kipaumbele kwa shughuli za uchaguzi.

Vilevile, tunaishukuru Serikali kwa kuiwezesha Tume kuwa na jengo la ofisi Dodoma ambapo sasa ndio makao makuu yake. Kwa namna ya kipekee tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuipatia Tume ya Taifa ya Uchaguzi jengo la ofisi ambalo baada ya ukarabati wake kukamilika limetumika na litaendelea kutumika kwa shughuli za uchaguzi kwa upande wa Zanzibar. Aidha, tunatoa shukrani kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa ushirikiano iliotoa kwa NEC katika kutekeleza majukumu yake upande za Zanzibar.

***Mheshimiwa Rais;***

Vyama vya siasa nchini ni wadau wakuu wa michakato ya uchaguzi, Tume inatumia nafasi hii kuvishukuru vyama hivyo kwa ushirikiano waliotoa kwa njia mbalimbali pale walipohitajika hususan kwenye kamati mbalimbali muhimu za uchaguzi. Kundi lingine ni taasisi na asasi za kiraia ambazo zilishiriki kikamilifu katika maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye utazamaji wa uchaguzi, kutoa elimu ya mpiga kura na kuwa washauri kupitia kamati za uchaguzi ambazo walikuwa ni wajumbe.

Tume pia, inashukuru makundi maalum katika jamii hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kushiriki kwao katika michakato ya uchaguzi kwa mfano, wawakilishi wa watu wenye ulemavu wa kuona walishirikiana bega kwa bega na Tume kuhakikisha majalada ya nukta nundu yanapatikana kwa ubora ili kuwawezesha wasioona kupiga kura wenyewe bila usaidizi.

Haya yote yasingewezakana kufanyika bila ya ushiriki wa wadau muhimu sana wa uchaguzi ambao ni wapiga kura. Tume inatumia fursa hii kuwashurukuru wapiga kura wote waliojitokeza siku ya kupiga kura, pia na wananchi wa Tanzania ambao walihakikisha utulivu na amani vinakuwepo nchini wakati wote wa uchaguzi.

***Mheshimiwa Rais;***

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, Tume inaendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kutenga muda wako siku ya leo ili uweze kupokea taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Tunakutakia kila la heri katika jukumu la kuiongoza nchi yetu katika nyanja zote ikiwemo hii ya kuinua, kuikuza na kuilinda demokrasia ya nchi yetu.

Baada ya kusema haya, nichukue fursa hii kwa heshima na taadhima kuwasilisha na kukabidhi taarifa ya uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani ya mwaka 2020.

***Mheshimiwa Rais;***

Naomba kuwasilisha.

Jaji wa Rufaa (Mst.) Semistocles. S. Kaijage

**MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA UCHAGUZI**